# UDADIS WA NAMNA BORA YA KUTUMIA MTINDO KATIKA UTUNZI WA FASIHI ANDISHI: MFANO WA RIWAYA YA UTENGANO.

**NA**

**KAVUMA MUHAMMAD ABASI**

**21/U/24041/PS**

**TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUKAMILISHA BAADHI YA MASHARTI YA DIGRII YA KWANZA (BARS) (KISWAHILI) YA CHUO KIKUU CHA MAKERERE**

**SEPTEMBA 2024**

**UTHIBITISHO**

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma tasinifu hii yenye kichwa: UDADIS WA NAMNA BORA YA KUTUMIA KIPENGELE CHA MTINDO KATIKA UTUNZI WA FASIHI ANDISHI: MFANO WA RIWAYA YA UTENGANO *na* anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu cha Makerere kwa ajili ya Kukamilisha Masharti ya Digrii ya Sanaa (BARS) (Kiswahili) ya Chuo Kikuu cha Makerere

......................................................................

Mwl. Nelson Nsereko

Tarehe:

8-8-2024

......................................................................

## IKIRARI

Mimi, **KAVUMA MUHAMMAD ABASI**, ninathibitisha kwamba tasinifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine kwa ajili ya kutunukiwa Digrii kama hii au Digrii nyingine yoyote.

Saini

KMAbasi ...................................

Tarehe

08 - 08 - 2024 ...................................

## Digitisation and Self-Archiving Consent Agreement: Theses

**Agreement between Makerere University & Students (Authors of Theses / Dissertations / Reports)**

1. The author is a student of Makerere University and author of the thesis / dissertation entitled: UDADISI WA NAMNA BORA YA ~~MATUMIZI~~ KUTUMIA MTINDO KATIKA UTUNZI WA FASIHI ANDISHI: MFANO WA RIWAYA YA UTENGANO.

2. The author grants to the University:
   a. The right to deposit the electronic version of the Thesis / Dissertation into Makerere University Institutional Repositories (Mak IR) or (Mak UD); and
   b. The right to store the thesis / dissertation in Mak IR / Mak UD and make it permanently available to the general public via the Internet at no cost to the general public after a grace period (if any is specified). Choose one of the two options below:
   c. The Author may opt for immediate open access to the public Immediate open access
   d. Or Restrict access indefinitely or for the specified number of years: ....................

3. The author warrants that to the best of the authors knowledge and belief:
   a. The thesis / dissertation is an original work;
   b. The author is the owner of all the intellectual property in the thesis / dissertation; or
   c. The Author is entitled to deal with the intellectual property in the thesis / dissertation by publishing it on the Internet
   d. The Author has the right, power and authority to enter into this Agreement and to grant the University the rights contained in this Agreement; and
   e. The University's use of the thesis / dissertation pursuant to this Agreement will not infringe the intellectual property rights of any third party.

4. The Author acknowledges and agrees that the University is not responsible or liable for any breach of the intellectual property rights in the thesis / dissertation, in particular any breach of copyright, as a result of the use of the thesis / dissertation pursuant to this Agreement.

5. The University acknowledges that the rights granted by the Creator in clause 2 of this Agreement, do not cause any transfer or assignment of any proprietary rights in the intellectual property in the article to the University.

Signed by the Author as confirmation that the Author has read and accepted the terms of this Agreement:

Name: KAVUMA MUHAMMAD ABASI

College/School: ~~COLLEG~~ SLLC Department: Languages

(Tick) Type of Degree: (Undergraduate ✓ / PGD / Masters / PhD), Reg. No.: 21/U/24041/PS

Tel No.: 0703636044 E-Mail: akavu361@gmail.com

Signature: KMAbasi Date: 26/05/2025

Supervisor's endorsement: ____________________

**MakIRs Policy**

## TABARUKU

Tasinifu hii ninaitabaruku kwa wazazi wangu, kwanza kabisa kwa marehemu mama yangu mzazi Rahma Kiyimba. Mama ndio chuo cha kwanza na cha msingi Zaidi kuliiko vyote kwani vingine vyote hujengwa juu ya msingi wa malezi yake. Alifanya jitihada za juu chini kuona kwamba ananijenga kuwa mtu aliyestarabika na kuadabika, mvumilivu na asiyekata tamaa. Isitoshe, aliniunga mkono katika safari ya maisha yangu yote ya kimasomo kuanzia chekechea hadi kumaliza senkondari ambapo aliiaga dunia. Alipangalo mungu binadamu hawezi kulipanguwa, ningependa sana anishuhudie wakati nikipewa cheti hiki cha shahada ya kwanza ila muumba ashakata shauri la mwisho. Hali kadhalika sitoshindwa kuitunuku kazi hii katika heshima yake. Siwezi kumpa malipo kamili kwa mhanga aliojitoa ila namomba mwenyezi mungu ampe Janatul Firdaus kwa wema alionitendea.

Mwisho kabisa ninaitabaruku kazi hii kwa familia ya Kigamboni, Dar es salaam kwa msaada walionipa katika kujifunza lugha hii ya Kiswahili na kunijengea mazingira stahiki kwa ajili kupata umahiri wa lugha. Hususan ninamshukuru marehemu baba Hashim Saiboko kwa kunipokea kifua wazi na kunielimisha ipasavyo hadi hatua ya kumaliza sekondari ambapo aliiaga dunia. Pia ninamshuru mama al maarufu Bii Khadija kwa malezi bora na msaada na ushauri alionipa katika kujifunza lugha. Isitoshe, ninamshukuru kaka Samora na Mama Nuran kwa kunipa huduma za mwanzo kabisa za elimu ya lugha ya Kiswahili kupitia wajanja wao wawili yaani, Nuran na Naira. Aidha, Shukran za dhati kwa baki ya kaka na dada zangu wote katika nyumba ya Saiboko. Hususan waalimu wangu wa kwanza Ridhwan Lenga na Saadi, kisha Asma, Fahima, Rahma na Wabichwa. Kwangu nyote ni waalimu na ndugu wa dhati ya nafsi yangu. Nawaombea Allah awalipe kila la kheri hapa duniani na kesho akhira.

## SHUKRANI

Kabla ya yote, nitaanza na kumshukuru mwenyezimungu kuniwezesha kufikia hatua hii ya safari ya masomo iliyojaa vikwazo na changamoto mbalimbali. Kwa uwezo na huruma zake mungu nimeweza kuzikabili changamoto zote hizi na mwisho wa siku kufikia hatua ya kuhitimisha shada ya kwanza. Pia ninamshukuru mungu kuniwezehsa kufikia hatua hii nikiwa katika hali ya uzima wa kiafia na miongoni mwa wachache waliofanikiwa kutimiza vigezo vya shahada hii.

Baada ya kumshukuru mungu, ninawashukuru wazazi wangu kwa malezi bora waliyonipa katika nyanja zote za maisha. Hususan ninamshukuru baba kwa kupokea jukumu la uzazi kwa kifua wazazi na kulitekeleza pasi na kusita kwa aina yote ile. Pia ninamshukuru kunielimisha kuanzia hatua za mwanzo hadi kukamilisha shahada ya kwanza. Ninamshukuru marehemu mama yangu kuwa kichochezi cha furaha na matumaini hasa katika nyakati ngumu. Mungu awalipe kila la kheri hapa duniani na ssskesho akhira.

Ninamshukuru msimamiizi wangu Mwl. Nelson Nsereko kwa kujitoa kunisimamia na kuvumilia makossa yangu na usumbufu uliojitokeza katika utekelezaji wa kazi hii toka mwanzo hadi mwisho. Pia ninamshukuru kwa maarifa, maoni na usahihishaji tofauti tofauti uliofanya katika kazi yangu jambo ambalo limeniwezesha kufanikiwa kukamilisha kazi hii.

Ninawashukuru waalimu wangu wote kwa mafunzo yote waliyonipa katika muda wa miaka mitatu ya kosi hii. Kwa kweli haikuwa kazi rahisi ila huduma ya mmeitoa pamoja na changamoto zote zilizoambatana na mchakato mzima. Hususan ninawashukuru walimu wangu wa Kiswahili, Kama vile Dkt. Mtungi Boaz, Dkt. Masengo Innocent, Mwl. Nsereko Nelson na wengine ambao sijaweza kuwataja kwa sababu moja ama nyingine. Pia shukrani za dhati kwa walimu wangu wa somo la falsafa kama vile Prof. Edward Wamala, Prof. Shimiyyu, Dkt. Jimmy Spire Sssentongo, Mwl. Siriyako Vincent na wengine.

Ninawashukuru wanafunzi wenzangu kwa umoja na mshikamano waliotoa kupitia mijadala ya kimasomo na mazoezi ya kiutafiti ya kozi. Hususan wale wa Kiswahili kama vile kiongozi wa darasa Nabaasa Viola, Akampulira Franklin, Mbabazi Jenifer na Aziza Muhammad. Kisha wale wa falsafa kama vile Aromorowt Judith, Nakazibwe Rebecca na Kakembo maarufu kwa Dj. Kakes.

Mwisho kabisa ninaishukuru familia ya Ubungo Islamic kwa umoja na mshikamano waliwonipa katika safari yangu ya kujifunza Kiswahili. Hususan shurani za dhati ziende kwa Suleiman Omar al maarufu Sele Mandondo, Hamadi Mbarouk al maarufu Gwanta na

Mwanangu Macho na wengine. Huenda msitambue ukubwa wa mchango wenu katika safari yangu ila Allah mjuzi wa kila kitu awazidishie wema juu ya wema kwa ukarimu mlionionesha.

# IKISIRI

Tasnifu hii inahusu kazi ya utafiti iliyoandikwa juu ya mada ya UDADIS WA NAMNA BORA YA KUTUMIA MTINDO KATIKA UTUNZI WA FASIHI ANDISHI: MFANO WA RIWAYA YA UTENGANO. Tasnifu hii ni mojawapo ya vigezo mbalimbali ambavyo wanafunzi sharti watimize kabla ya kupata shada yao ya kwanza. Kazi imechunguza suala zima la matumizi bora ya mtindo kipengele mojwapo cha fani ya kazi ya fasihi andishi. Mtindo umezingatiwa katika kazi hii kwa sababu nyingi kati ya kazi za fasihi andishii hukosa hadhira na hivyo kufa mapema kwa sababu ya makossa ya kimtindo. Lengo kuu la kazi hii ni kubaini namna ambavyo wandishi wa kazi za fasihi andishi hutumia kipengele cha mtindo kuwasilisha kazi zao. Lengo hili limeendewa kupitia hatua mahususi tatu yaani, kwanza kabisa ni kutoa mifano ya aina za mitindo inayotumiwa katika uwasilishaji wa fasihi andishi, pili tulionesha namna bora ya kutumia mitindo hii katika kutunga kazi za kifasihi na mwisho kabisa kazi ulijadili baadhi ya makossa ambayo hutendwa na watunzi wa fasihi andishi wanapotumia mitindo mbalimbal. Utafiti huu umetumia mbinu ya upekuzi wa yaliyomo. Yaani, tunaweza kusema upekuzi uliofanywa hapa ni ule wa kimaktaba ambapo marejeo mbalimbali yamepitiwa hasa riwaya ya *Utengano* (1980). Utafiti umegundua kwamba makossa mengi yanayofanyika katika matumizi ya mtindo hupatikana katika kazi nnyingi za wandishi chipuzi. Jambo hili tumelibaini kupitia kutizama kazi yake ya *Utengano* (1980) ambayo ni miongoni mwa kazi alizozitoa mwanzoni na kuiliganisha na zile za hivi karibuni kama vile *Dunia Yao* (2006), tunaona kwamba pamoja na kuwa mwandishi huyu anadhihirisha ustadi mkubwa wa umilisi wa lugha, ipo tofauti kubwa kati ya uchaguzi wa msamiati kati ya riwaya hizi mbili ambapo kuna umakini mwingi uliotumika katika ile ya *Dunia Yao* (2006) ukilinganisha na ile ya *Utengano* (1980). Kwa muhtasari tunaweza kusema kwamba mtindo ni kipengele amabacho hutambulisha kiwango cha ufundi wa mtunzi kwa hadhira na ipo haja kubwa ya watu kuelimishwa juu ya namna bora ya kukitumia ili kuepukana na makosa ya kizembe yanayorudisha nyuma maedeleo ya fasihi. Hivyo basi, utafiti huu unapendekeza kwamba ipo haja kubwa ya kutizama upya matumizi ya vipengele vingine vya kazi ya fasi hasa vile vya fani kwa sababu bila ya umbo la nje kuboreshwa, la ndani pia haliwezi kuboreshwa.

**YALIYOMO**

YALIYOMO

UTHIBITISHO ........ ii

IKIRARI ........ iii

TABARUKU ........ v

SHUKRANI ........ vi

IKISIRI ........ viii

YALIYOMO ........ ix

SURA YA KWANZA ........ 1

USULI NA UTANGULIZI WA UTAFITI ........ 1

1.2 Usuli wa utafiti ........ 1

1.3 Tatizo La Utafiti ........ 2

1.4 Malengo ya Utafiti ........ 3

1.4.1 Lengo Kuu ........ 3

1.4.2 Malengo Mahususi ........ 3

1.5 Maswali ya Utafiti ........ 3

1.6 Sababu ya Kuchagua Mada ........ 3

1.7 Mchango wa Utafiti ........ 3

1.8 Changamoto za Utafiti na Utatuzi Wake ........ 4

1.9 Hitimisho ........ 5

SURA YA PILI ........ 6

MAPITIO YA MANDISHI ........ 6

2.0 Utangulizi ........ 6

2.1 Dhana ya Mtindo na Matumizi yake katika Uandishi wa Riwaya ........ 8

2.3 Msingi Wa Nadharia ........ 9

2.3.1 Utangulizi ........ 9

2.3.2 Nadharia Ya Utafiti ........................................................................................ 9
2.3.4 Viwango Vitakavyotumika Katika Utafiti ........................................................ 12
2.3.5 Hitimisho ........................................................................................ 13
SURA YA TATU ........................................................................................ 14
MBINU ZA UTAFITI ........................................................................................ 14
3.1 Utangulizi ........................................................................................ 14
3.2 Mkabala wa Utafiti ........................................................................................ 14
3.3 Usampulishaji ........................................................................................ 15
3.4 Mbinu za Utafiti ........................................................................................ 15
3.4.1 Upekuzi wa Yaliyomo ........................................................................................ 15
3.5 Vifaa Na Zana Za Utafiti ........................................................................................ 15
3.5.1 Vitabu ........................................................................................ 16
3.5.2 Makala Pamoja Na Majarida ........................................................................................ 16
3.5.3 Daftari La Kuchambulia Data Na Kunukuu Mambo Muhimu ........................................ 16
3.6 Uchanganuzi Data ........................................................................................ 16
3.7 Hitimisho ........................................................................................ 16
SURA YA NNE ........................................................................................ 17
MATOKEO YA UTAFITI ........................................................................................ 17
4.1 Utangulizi ........................................................................................ 17
4.2 Mitindo ya Uwasilishaji Ujumbe wa Kazi za Utanzu wa Riwaya. ........................................ 18
4.2.1 Aina za Mitindo ya Uwasilishaji wa Kazi za Fasihi ........................................ 18
4.2.2 Matumizi ya Lugha ........................................................................................ 19
4.2.3 Mtindo Wa Dayalojia ........................................................................................ 21
4.2.4 Mtindo Wa Barua ........................................................................................ 22
4.2.5 Mtindo wa Nyimbo au Ushairi. ........................................................................................ 22
4.2.6 Mtindo wa Ukuzaji wa Wahusika. ........................................................................................ 24

4.2.7 Namna ya Usimulizi ........................................................................................25
4.2.8 Ubadilishaji Wa Hati Au Mfumo Wa Herufi..................................................................26
4.3 Namna ya Kutumia Mitindo ya Uwasilishaji wa Kazi .....................................................26
4.3.1 Uchaguzi wa Mada. ..........................................................................................27
4.3.2 Kusoma na Kuelewa Mada ...................................................................................27
4.3.3 Kuoanisha Mandhari na Toni ................................................................................27
4.4.0 Makosa ya Utunzi wa Riwaya ...............................................................................28
4.4.1 Unganganizi wa Mtindo Mmoja ..............................................................................28
4.4.2 Waandishi Chipukizi Kuigaiga ...............................................................................28
4.4.3 Matumizi ya Lugha ...........................................................................................29
4.4.4 Kutofahamu Hadhira...........................................................................................29
4.4.5 Kutumia Maneno Yasiyo Sahihi ..............................................................................29
4.4.6 Utumiaji Lugha Ya Matusi ....................................................................................29
4.4.7 Kutumia Mitindo Iliyopitwa Na Wakati .....................................................................30
SURA YA TANO ........................................................................................................31
HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .........................................................................................31
5.1 Utangulizi.........................................................................................................31
5.2 Muhtasari wa Utafiti ..........................................................................................31
5.3.1 Haja ya Kuangalia Matumizi Bora ya Vipengele Vingine .............................................32
5.4 Hitimisho..........................................................................................................32
Marejeo ..................................................................................................................33

# SURA YA KWANZA

# USULI NA UTANGULIZI WA UTAFITI

## 1.1 Utangulizi

Utafiti huu ulilenga kuchunguza namna ambavyo wandishi wa riwaya hutumia kipengele cha mtindo kutofautisha kazi zao na zile za wandishi wengine. Hii ni kwa sababu katika utunzi wa kazi ya riwaya mwandishi hupitia kipengele hiki kudhihirisha ubunifu wake binafsi. Yaani, hadhira inaweza kubaini kwamba huenda kazi Fulani ikawa ya msanii au mtunzi Fulani kutokana na matumizi ya utaratibu Fulani katika kazi hiyo. Hivyo basi, tunaweza kusema kusema kwamaba utafiti huu ulilenga kuchunguza juu ya namna bora ya kutumia kipengele cha mtindo. Katika kushughulikia mada ya utafiti tulijadili mambo ya kuzingatia tunapotumia mitindo mablimbali na makosa yanayofanyikwa na wandishi. Utafiti huu ni utafiti wa maktabani. Hapa riwaya ya *Utengano* (1980) na Said Ahmed Mohamed ilichunguzwa kama rejeo la kiada na kazi watafiti na wasomi wengine zilichunguzwa kama marejeo ya ziada.

## 1.2 Usuli wa utafiti

Kabla ya kuingia katika kiini cha sehemu hii nitafafanua kwanza dhana muhimu tatu yaani fasihi, fani na mtindo ili kuondoa utata wa aina yoyote ile.

Kwanza kabisa, fasihi kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali akiwemo Wamitila (2003) na wengine yapo maafikiano kwamba fasihi ni kazi ya kubuni ambayo hutengenezwa kwa kutumia lugha na uhalisia wa maisha ya watu wa jamii fulani na huathiriwa na mabadilko ya kijamii.

Fani kwa upande mwingine ni umbo la nje la kazi ya kifasihi ambalo hudhirika kwa hadhira pasi na kutegemea fikra zao kama vile vipengele vya kimaudhui.

Mtindo ni kipengele mojawapo ya vile vya fani ya kazi ya fasihi ambcho kimefafanuliwa katika namna mbalimbali kama ifuatavyo: Senkoro (1982) anasema mtindo katika kazi ya fasihi ni ile namna ambayo msanii hutunga kazi hiyo na kuipa sura ambayo kifani na kimaudhui huainisha kanuni au kawaida zilizofuatwa (za kimapokeo) ama ni za kipekee. Anaendelea kusema, mtindo ni upangaji wa fani na maudhui katika kazi ya fasihi kwa njia ambayo hutokeza au huonyesha nafsi na labda upekee wa mtungaji wa kazi hiyo.

Kazi nyingi za kiutafiti zimetolewa na watafiti au wasomi mbalimbali hapo nyuma juu ya mada ya mtindo au kazi za mwandishi Saidi Ahmed Mohamed. Kwa mfano, Motanya, M.M;

Kisurulia, E; Sawe, S (2021) wanasema katika kazi yao iliyochapishwa katika jarida la IAJSSE kwamba, Utafiti huu unaonyesha jinsi aina mbalimbali za ukiushi wa kiisimu zilivyotumiwa katika kuendeleza mtindo wa kazi zilizoteuliwa. Aina za ukiushi ambazo zimeshughulikiwa ni ukiushi wa kifonolojia, wa kimofolojia, ukiushi unaotokana na athari za lugha ya kwanza, wa kisarufi (ukiushi wa kisintaksia na kisemantiki) na ukiushi wa kiisimu matini.

Pia kwa mujibu wa Mtungu (2019) Kitaaluma, utafiti huu umetoa mchango wa mawazo mapya kuhusu matumizi ya ulemavu katika kazi ya fasihi kwa lengo la kuihamasisha jamii kuhusu masuala mbalimbali. Aidha ni msingi muhimu wa kuangazia mwelekeo tofauti wa uhakiki wa suala la ulemavu tofauti na tafiti nyingi ambazo zimezingatia upungufu na haki za watu wenye ulemavu. Utafiti huu umedhihirisha kuwa kuna mbinu zaidi na za kipekee zinazotumika kama mtindo katika kazi za fasihi bali na zile zinazohusiana moja kwa moja na tamathali za lugha; na hivyo basi kuchochea uchunguzi zaidi.
Licha ya sampuli ya bahari ya mifano iliyotolewa hapo juu zipo tafiti nnyingi zimetolewa zikisawiri mada ya utafiti huu lakini ilikuwa bado kupatikana kazi ambayo hususan inajadili au kuchunguza namna ambavyo wasanii wa riwaya kama vile Mohamed wanafinyanga kipengele cha mtindo kwa ustadi na ufundi ili kuzalisha ule msisimko unaojitokeza katika kazi zao na hivyo basi utafiti ulijikita katika kuvumbua kiini cha mafanikio hayo.

### 1.3 Tatizo La Utafiti

Utafiti mwingi umetangulia kuafanywa juu ya mada ya mtindo lakini nnyingi kati ya tafiti tangulizi zimeangalia namna mtindo unavyotumika katika kazi za wandishi mbalimbali. Mfano, kwa mujibu wa Motanya, M. M, Kisurulia, E na Sawe S (2021) wanasema Utafiti huu unaonyesha jinsi aina mbalimbali za ukiushi wa kiisimu zilivyotumiwa katika kuendeleza mtindo wa kazi zilizoteuliwa. Aina za ukiushi ambazo zimeshughulikiwa ni ukiushi wa kifonolojia, wa kimofolojia, ukiushi unaotokana na athari za lugha ya kwanza, wa kisarufi (ukiushi wa kisintaksia na kisemantiki) na ukiushi wa kiisimu matini. Bado kupatikana kazi ya kiutafiti ambayo inaelekeza juu ya namna mwafaka ya kutumia mtindo katika kuwasilisha ujumbe katika kazi ya kifasihi. Hivyo basi, utafiti huu ulidadisi namna bora ya kutumia mtindo kaika kuwasilisha ujumbe katika kazi za fasihi andishi kwa kutumia riwaya ya Utengano (1980) kama rejeo la kiada.

### 1.4 Malengo ya Utafiti

#### 1.4.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kudadisi namna ambavyo mitindo ya uwasilishaji wa fasihi andishi hutumika na waandishi.

#### 1.4.2 Malengo Mahususi

(i) Kubaini mitindo ambayo Mohamed (1980) ametumia kuwasilisha kazi yake

(ii) Kufafanua kwa nini lazima kazi ipwekeke iwapo mitindo itatumika katika namna stahiki.

(iii) Kufafanua kwa nini baadhi ya kazi za kisanaa hukosa mvuto wa kiubunifu.

### 1.5 Maswali ya Utafiti

(i) Waandishi wa riwaya hutumia mitindo gani katika kuwasilisha ujumbe wao kwa hadhira zao lengwa?

(ii) Mitindo ya uwasilishaji riwaya inatumika je?

(iii) Ni makosa gani yanayofanywa na baadhi ya wandishi wa riwaya katika utumiaji wa mitindo?

### 1.6 Sababu ya Kuchagua Mada

Uchaguzi wa mada hii kwa upande mkubwa umetegemea uwezo wangu binafsi wa kuchangia katika kuziba pengo la elimu ya Kiswahili ambalo kupata umakini wa baki ya wasomi wa ulimwengu wa Kiswahili. Hivyo basi, ili niweze kutoa kazi ambayo ni ya kifundi sina budi kuchagua mada ambayo ipo ndani ya uwezo wangu. Pia sababu nyingine ya kuchagua mada hii ni urahisi na hili ni jambo ambalo nimezingatia kwa sababu kufanya jambo ambalo halikupi wakati mgumu ni sababu ya kufanya kazi kwa urahisi na hivyo basi kuboresha matokeo.

### 1.7 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa na michango mbalimbali ila hapa tutatoa ile michango mikuu tu na sio kila mchango. Bila shaka mchango mkuu unaotarajiwa kutolewa na utafiti huu ni kuziba pengo utafiti linaloshughilikiwa na utafiti huu. Mchango mwingine utakaoletwa na utafiti huu ni kuongeza kwenye hazina ya mandishi ya elimu ya Kiswahili na hivyo basi kukuza lugha ya Kiswahili na fasihi ya Kiswahili kwa ujumla. Pia mchango mwingine ni kwamba utafiti huu utaongeza idadi ya mijadala katika fani mbalimbali za elimu ya lugha ya Kiswahili na hivyo kukuza ustadi na umahiri katika wataalamu wa lugha ya Kiswahili. Mwisho kabisa utafiti huu

utaongeza kwenye idadi ya wasomi wa lugha ya Kiswahili waliothibitishwa kwa sababu ni kigezo cha mwisho katika kukamilisha shahada ya kwanza ya digirii ya Kiswahili.

### 1.8 Changamoto za Utafiti na Utatuzi Wake

Kila mchakato duniani lazima uwe na changamoto zake hivyo basi na zoezi la utafiti lazima liwe na changamoto zake ambazo zinatofautiana kutoka mtafiti mmoja hadi mwingine. Nilikumbwa na changamoto tofauti-tofauti kama ifuatavyo;

Kuchagua mada ya utafiti. Hapa nilipata wakati mgumu kupata mada mafaka ambayo inaweza kushughulikiwa kiufundi na amabyo haijawahi kushughulikiwa hapo kabla na ambayo itakuwa rahisi kiasi cha kwamba nitaweza kuishughulikia kwa ustadi na kutoa kazi faafu. Changamoto hii ili tatuliwa kwa namna ifuatayo; kwanza kabisa niliamua kuweka umakini wangu kwenye matawi makuu mawili ya elimu ya lugha ya Kiswahili nikafanya tathmini yangu na mwisho wa siku nikaamua kuenda na mada fasihi na na katika fasihi nikaamua kuchambua kazi ya riwaya na hivyo basi nikachagua riwaya ya Utengano.

Kupata kiunzi cha nadharia kwa ajili ya mada yangu. Nilitatizika sana kupata nadharia mwafaka ambayo ingefaa kuchambulia kazi ya riwaya na pia kufafanulia matumizi ya mitindo mbalimbali. Changamoto hii ilitatuliwa kama ifuatavyo; Utatuzi wa changamoto hii haukua na njia makato na hivyo basi, ili nibidi kupitia kazi mbalimbali za watafiti watangulizi ambapo baadae nilikuja kuchagua nadharia ya umitindo kwa sababu ndio iliyokuwa na sifa stahiki kwa ajili ya utafiti wangu.

Upatikanaji wa marejeo. Hususan yale ya ziada yalikuwa magumu sana kupatikana kwa sababu nnyingi kati ya kazi zilizo chapishwa mtandaoni ni za kulipia na sio za bure. Katika utatuzi wa changamoto hii, nilianza na kuuliza maswali kwa wanaonizidi maarifa ambapo mwisho wa siku nilielekezwa ipasavyo. Marejeo mengine nimeyapata kupitia kuyalipia na mengine nimeyapata kupitia upekuzi wa kazi tangulizi.

### 1.9 Hitimisho

Sura hii inatoa muhtasari wa mchakatomzima wa utafiti na namna ambavyo ulitekelezwa. Kwa mfano kupitia kipengele cha utangulizi, usuli, na tatizo la utafiti tunapata ufafanuzi wa mada ya utafiti na sababu kwa nini kulikua na haja ya kushughulikia mada hii. Kwa upande l kupittia kipengele cha malengo ya utafiti na maswali ya utafiti surah hii tunaona namna ambavyo zoezi zima la uchambuzi wa mada ya utafiti lilivyotekelezwa. Pia sura hii inazungumzia juu ya sababu ambazo zilipelekea uchaguzi wa mada ya utafiti. Mwisho kabisa surah ii inajadili matatizo ambayo yaliukumba mchakato mzima wa utafiti na namna ambayo yalitatuliwa.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MANDISHI

## 2.0 Utangulizi

Sura hii itajadili juu ya mambo makuu mawili. Jambo la kwanza ni mapitio ya mandishi ya wataalamu waliotangulia katika kutafiti mada ya utafiti huu. Jambo la pili ambalo litajadiliwa ni kiunzi cha nadharia ambayo ilitumika kuongoza utekelezaji wa utafiti huu.

## 2.1 Machache Kuhusu Mwandishi

Sad Ahmed Mohamed alizaliwa mwaka 1947 katika mtaa wa Limbani, Wete Pemba tarehe kumi na mbili Disemba. Maisha yake ya utoto aliyaishi katika mji wa Unguja ambako alisoma juzuu na Mas-haf katika madrasa na kuidhinishwa kusoma Qur an. Skuli ya Darajani iliyopo mpakani kati ya ng'ambo na Mji Mkongwe aliweka unyayo wake katika safari ndefu ya kuisaka elimu . Alipelekwa shule ya sekondari King George VI baada ya ufaulu wake wa mzuri mitihani ya darasa la saba.

Alijiunga katika Chuo cha Uwalimu Nkrumah ndani ya mwaka 1966. Kati ya mwaka 1969 na 1974 akaajiriwa na kuanza kufundisha katika shule mbalimbali kisiwani Pemba. Said alifundisha masomo ya Sayansi na hesabu na sio lugha. Hamu ya kujiendeleza kielimu ikamsukuma na kujiandaa. Mwaka 1976 alijikuta yupo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam anachukua masomo ya Kiswahili, Fasihi na Isimu, Fasihi kwa Kiingereza na Ualimu. Ufaulu wake katika daraja hii ulikua mzuri sana kiasi cha kwamba ulivvuta umakini wa wahadhiri wake wa chuo. Hususan Sigmund Brunner kutoka Ujerumani Mashariki aligundua mapema kipaji chake na kumshawishi aende Ujerumani kwa masomo ya juu. Bila ya kusita kwa namna yoyote ile, Said alipanda ndege hadi Ujerumani na kujiunga na Chuo Kikuu cha Karl Marx hapo Leipzig mwaka 1985.

Huko ujerumani, Said alisoma isimu na kwa wakati huohuo akafanya kazi ya ualimu wa Kiswahili kwa Wajerumani walio kuwa wakijifunza kugha ya kiswahili. Baada ya kumaliza shahada ya umahiri na ile ya uzamivu, alirudi nyumbani na kuanza kufundisha katika vyuo mbalimbali. Aliwahi kuwa mkurugenzi wa iliyokuwa Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni (TAKILUKI). Taaluma yake ya kufundisha na umahiri wake wa kuandika vikawa chanzo cha mvuto pamoja na umaarufu wake katika ulimwengu wa elimu ya Kiswahili. Vyuo na asasi za elimu zikawa zinapigana vikumbo kumwinda. Said alifundisha Nairobi, Kenya na baadaye

Japan, Osaka ambako alitunukiwa Uprofesa kabla kuhitimisha kufundisha huko Ujerumani katika Chuo Kikuu cha Bayreuth mwaka 1992. Hivi sasa amestaafu lakini Waswahili husema ujuzi hauzeeki. Chuo Kikuu cha Zanzibar kimemuomba afundishe kozi za Uzamivu.

Kipaji chake cha uandishi ni cha urithi wa mama yake ambaye alikuwa mtunzi wa nyimbo za papo kwa papo na mghani mashuhuri na mtambaji wa hadithi za Fasihi Simulizi.Mkaa na waridi haachi kunukia, Said alipata majazi ya mama tokea utotoni. Akiwa shuleni darasa la tano alianza kutunga hadithi na mashauri, mambo yaliyowavutia sana walimu wake. Shairi lililovutia zaidi ni like liitwalo 'Nimfuge Ndege Gani?' (1960) kuanzia hapo kalamu hakuiweka chini. Akaandika mashairi yaliyosomwa katika redio ya sauti ya Unguja siku hizo na sasa ni redio ya Shirika la Utangazi la Zanzibar (ZBC). Alitiwa moyo na kuraghabishwa na jozi ya walimu wake Mohamed Abdulla na Kindy Abubakar.

Mwandishi huyu alikuwa mchanga alianza kunyemelewa na umaarufu pale hadithi zake fupi zilipoanzwa kusomwa katika idhaa ya BBC na DW. Kuanzia mwaka 1976 kilipotoka kwa kishindo kitabu chake cha kwanza cha riwaya ya Asali Chungu hadi sasa ameandika jumla ya vitabu sitini na saba vikiwemo riwaya, Hadithi fupi, mashairi na heshima za lugha na Isimu. Vitabu vya hivi karibuni ni Babu Alipofufuka (2001), Dunia Yao (2006), Nyuso za Mwanamke (2010), Atamlilia Nani (2009), Vipawa vya Hasina (2009), Mkama Ndume (2013), Masikini Bibi Yangu (2009), Kimya Kimya, Mshetani Wamerudi. Riwaya hizi zina mwelekeo mpya wa usasa baadaye tofauti na riwaya kabla ya hizi. Riwaya na kazi nyengine za fasihi ni pamoja na Sikate Tamaa (2001), Kina cha Maisha (1984) na Jicho la Ndani (2000). Riwaya zake nyingine ni Posa za Bi Kisiwa (2007), Asali Chungu (1977), Dunia Mti Mkavu (1980), Kiza katika Nuru (1988) na Tata za Asumin (1990).

## 2.2 Dhana ya Mtindo na Matumizi yake katika Uandishi wa Riwaya

Profesa Saidi Ahmed Mohamed ameandika vitabu vingi (zaidi ya arubaini) vikiwemo vya riwaya, tamthiliya, ushairi na hadithi fupi na makala nyengine za kitaaluma. Mtafiti ameona kuna umuhimu mkubwa wa kufanya mapitio ya baadhi ya kazi tangulizi za wandishi wa upande wa riwaya ambao ndio mtafiti anaoushughulikia ili kuweza kubaini juhudi zake na uwandishi wake hususan kuhusu suala zima la matumizi ya mtindo.

Kitali (2011) alishughulikia fani katika tamthilia mbili, Pango na Mama Ee. Alichunguza jinsi wahusika wanawake walivyotumia lugha. Katika kipengele cha mtindo, aliangalia mbinu za lugha zilizoteuliwa na mwandishi kama zimemkuza ama kumdunisha mwanamke. Yeye alijikita katika fani na matumizi ya lugha iliyosimulia kazi hizo.

Ongarora (2007) alishughulikia "Mtindo katika „Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine". Alishughulikia mtindo kama matumizi ya lugha. Alihakiki ukiushi katika mpangilio wa nomino, vitenzi, vielezi, viunganishi na vihusishi katika sentensi. Tena aliangazia baadhi ya ukiushi wa kisemantiki na mbinu nyingine za lugha katika "Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine."

Ndung‟u (1996) katika tasnifu yake "Uhakiki wa Fani katika Riwaya za Katama Mkangi", alichunguza vipengele vya mtindo na kutathmini kufaa kwa matumizi yake. Pia alichunguza maudhui katika Ukiwa (1975), Mafuta (1984), na Walenisi (1995). Kazi yake ilitufaa katika uchanganuzi wa mtindo na wahusika japo ilitofautiana na yetu kwa sababu alitafitia kipengele cha ploti ambacho sisi hatukukitafiti.

Katutu (2013) alishughulikia "Mtindo katika „Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine‟ ya Said Mohamed". Alijikita katika matumizi ya msamiati na mtindo kwa misingi ya kisintaksia. Katika matumizi ya msamiati wa diwani hiyo alichunguza pia ukiushi katika baadhi ya kategoria za maneno; sentensi ndefu, fupi na nafasi ya uakifishaji katika sintaksia ya diwani yenyewe.

## 2.3 Msingi Wa Nadharia

### 2.3.1 Utangulizi

Kwa kuwa utafiti ni suala la kielimu, mtafiti hanabudi kuegemeza mchakato wa uchunguzi wake kwenye kazi za watafiti au wataalamu wabobezi wa fani pamoja na kiunzi cha nadharia ili kuepuka kufanana kama mjinga anayefanya mambo kwa mtindo wa kibubusa. Pia kiunzi cha nadharia lazima kiwepo ili kushawishi wasomi wake kupokea kazi yake kwa hadhi yake stahiki na sio mashindi kimzaha.

### 2.3.2 Nadharia Ya Utafiti

Wafula na Njogu (2007) wanasema, Nadharia ni jumla ya maelekezo yanayomsaidia msomaji au mhakiki kuifahamu kazi ya fasihi kwa kufuata utaratibu maalum.

Msokile (1993) anafafanua, Nadharia ni mawazo, mpango, mwongozo, maelezo, yaliyowekwa ili kusaidia kutatua au kutekeleza jambo fulani.

Massamba (2009:63) anasema, Nadharia ni taratibu, kanuni na misingi ambayo imejengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhumuni ya kutumiwa kama kielelezo cha kuelezea jambo.

Wamitila (2002) anaeleza, Nadharia za uhakiki ni muongozo unaomuelekeza msomaji na mhakiki kwenye vipengele vya msingi vya nadharia anayoitumia.

Kwa ujumla: Nadharia ni jumla ya maelekezo, taratibu, kanuni, misingi, mfumo uliorasmi, mwongozo na mpango unaotumiwa na mhakiki au mtafiti ili kumsaidia kuifanikisha na kutekeleza kazi yake ya fasihi katika kiwango cha ufanisi zaidi.

Kwa hakika kila nadharia huwa ni muhimu na yenye ubora na mapungufu yake.

Uteuzi wa nadharia bora inategemea uteuzi wa mtafiti kwa mujibu wa mada, malengo na maswali ya utafiti wake. Utafiti huu umekusudia kutumia nadharia ya Umitindo.

Katika utafiti wetu tulitumia nadharia ya Umitindo ambayo ina wataalamu wengi walioieleza kama: Geoffrey Leech (1969), Crystal na Davy (1969), Leech na Short (1981, 2007), Paul Simpson (2004) na wengine. Wataalamu hawa walieleza nadharia ya Umitindo ambayo ilituongoza katika utafiti wetu.

Ila nadharia ya umitindo iliasisiwa mwaka wa 1904 na Viktor Shyklovsky alipogundua kuwa lugha hutumika kwa njia inayofanya mambo ya kawaida kuonekana mapya. Leech (1969) anasema kuwa umitindo ni uhakiki na fasiri ya matini katika mtazamo wa kiisimu kama taaluma, unaofungamanisha uhakiki wa kifasihi na kiisimu ingawa haujisimamii kivyake. Msamiati mpana wa kimsingi katika uhakiki wa kifasihi hususan taswira, kinyume, kinaya,

kejeli, usambamba na jazanda hauwezi kufafanuliwa bila kurejelea dhana za kiisimu kama vile fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Umitindo huangazia matumizi ya dayolojia au mazungumzo yanayohusisha lafudhi zinazotambulisha maeneo ya kijiografia na lahaja za wazungumzaji wa eneo fulani, lugha elezi na sarufi kwa mfano sajili au rejista, sauti, aina za sentensi na kadhalika. Kimsingi, nadharia hii inaweza kuchunguza mtindo wa kinachosemwa au kuwasilishwa na jinsi kinavyowasilishwa. Nilitumia nadharia hii kwa sababu mwandishi Said Ahmed Mohamed kama ilivyo kawaida ya wandishi wengi, alitumia nadharia hii ndio bora zai mchanganyiko wa mitindo katika riwaya yake katika uwasilishaji wa ujumbe wake kwa hadhira yake.

Mtindo unaweza kuhusishwa na lugha ya maandishi, lugha ya kifasihi au isiyokuwa ya kifasihi ingawa kwa kawaida huwa unahusishwa na matini za kifasihi zilizoandikwa. Katika uandishi wa fasihi, istilahi “mtindo” hutumika kwa maana nyingi: Ni mazoea ya lugha kama wanavyosema Wana-umitindo (Crystal na Davy 1969). Wanasema tunaweza kuhusisha mtindo na mazoea ya matumizi ya lugha ya mtu binafsi au jamii-lugha, na hii ndiyo maana ambayo huwajia watu akilini wanapozungumza kuhusu mtindo wa uandishi wa mtu fulani, mtindo wa kuzungumza, wa kutoa hotuba hadharani, n.k.

Leech (1969) katika kitabu chake A Lingustic Guide to English Poetry, alisema yafuatayo kuhusu Umitindo:

Umitindo ni uhakiki na fasiri ya matini katika mtazamo wa kiisimu kama taaluma, unaofungamanisha uhakiki wa kifasihi na kiisimu ingawa haijisimamii kivyake. Msamiati mpana wa kimsingi wa uhakiki wa kifasihi hususan sitiari, taswira, kinyume, kinaya, kejeli, usambamba na jazanda hauwezi kufafanuliwa bila kurejelea dhana za kiisimu. Kwa hivyo, kama msingi wa kutumia taaluma za kifasihi na za kiisimu, Umitindo ni uwanja ambamo masuala haya hushughulikiwa. (TY) (uk 11)

Kulingana nasi vipengele vya kifasihi na kiisimu ni vigumu kutengenisha wakati wa uhakiki kwa sababu vinaingiliana. Mjadala mkubwa umekuwepo kuhusu neno “mtindo,” ingawa istilahi hii imetumiwa sana katika uhakiki wa fasihi na hasa Umitindo. Istilahi hii imetumiwa katika miktadha mipana. (Leech na Short 2007) wanaeleza sifa za kisanaa zinazopatikana katika fasihi kama taaluma. Wanaeleza kuwa nadharia hii huangazia umuhimu wa lugha katika kueleza maana ya kifasihi. Na pia hutumiwa kurejelea jinsi lugha inavyotumiwa katika muktadha fulani, na mtu fulani na kwa lengo fulani. Katika kitabu Style in Fiction, Leech na Short walishughulikia suala la mtindo katika kuchanganua matini za fasihi kisayansi kama tutakavyoeleza baadaye.

Kulingana na Leech na Short, malengo ya stadi za Umitindo ni fasihi pamoja na maumbo mengine ya matini zilizoandikwa katika nyanja za fasihi, matangazo ya biashara, utamaduni, siasa au dini. Umitindo hujaribu kubainisha kanuni za kuelezea uteuzi uliofanywa na mwandishi
katika matumizi yake ya lugha kuhusu mambo ya kijamii, utoaji na upokeji wa maana, uhakiki wa kidiskosi na wa kifasihi. Zaidi walitaja kuwa Umitindo huangazia matumizi ya dayolojia au
mazungumzo yanayohusisha lafudhi za kimaeneo na lahaja za wazungumzaji, lugha elezi na sarufi k.m sauti, urefu wa sentensi na rejista.
Dhana ya mtindo ilielezwa zaidi na mwanaisimu wa Kiswisi Ferdinand De Saussure (1983) ambaye alioanisha taaluma ya Fasihi na ya Isimu kwa kutofautisha dhana ya "langue" na "parole" katika lugha au "langage" kama alivyoeleza Saussure, "langue" ni utaratibu wa kanuni za lugha zinazojulikana na wazungumzaji wa lugha husika. Yaani, ni mfumo wa lugha ya jamii inayohusika. "Parole" ni matumizi ya utaratibu au kanuni za lugha ya mzungumzaji binafsi. Ni uteuzi wa kanuni ambazo msemaji huzitumia katika uandishi na uzungumzi wake. Kwa hivyo, mtindo ni kama "Parole" kwa kuwa ni uteuzi kutoka katika utaratibu wa kanuni zilizoko za lugha. Kwa muhtasari, lugha inayojulikana na wazungumzaji yaani "langage" inaundwa kutokana na kanuni za lugha (langue) pamoja na matumizi yake katika mazungumzo na maandishi (parole).

**2.3.3 Sura Tofauti za Nadharia ya Umitindo** Nadharia ya Umitindo ina viwango ambavyo mchanganuzi wa matini ya kifasihi anahitaji
kuvizingatia ili kutekeleza uhakiki kwa njia ifaayo. (Leech na Short 2007) waliorodhesha aina za ukiushi wa kaida za matumizi ya lugha ambayo hutokea katika mtindo wa kazi za kifasihi. Viwango hivi vya ukiushi ni:

(i) Ukiushi wa kimsamiati/kileksia.

(ii) Ukiushi wa kisarufi.

(iii) Ukiushi wa kilahaja.

(iv) Ukiushi wa sajili/rejista.

(v) Ukiushi wa kifonolojia.

(vi) Ukiushi wa kimaandishi/kigrafolojia.
(vii) Ukiushi wa kimapisi/kihistoria
(viii) Ukiushi wa kisemantiki. (uk 120)

Kuna viwango vingi muhimu vya kuchunguzwa katika matini kwa kutegemea nadharia ya Umitindo kama wanavyoeleza Leech na Short (2007) na pia Simpson (2004). Maoni ya waasisi hawa yameungwa mkono na Wamitila (2008) ambaye anasema kuwa:

> Nadharia ya Umitindo inajikita kwenye uchunguzi wa lugha kwa kiasi kikubwa. Uchunguzi huu wa lugha unapania kubainisha ubunifu uliopo kwenye lugha hiyo na kwa kuutekeleza kwa undani unasaidia katika uelewekaji wa matini au kazi za kifasihi. Wamitila anaendelea kusema, maarifa yanayotokana na isimu hutumiwa ili kubaini sifa za kimtindo za kazi au matini ya kifasihi. Sifa hizi zinaweza kuwa za kifonolojia (ruwaza za sauti, vina, mizani), kisintaksia (miundo ya sentensi, aina ya sentensi), kimsamiati (maneno dhahania na maneno dhabiti, kuwepo na idadi ya nomino, vielezi, vivumishi n.k.) na kibalagha (matumizi ya tamathali za usemi, urudiaji na mbinu za urudiaji huo, jazanda) (uk.115)

### 2.3.4 Viwango Vitakavyotumika Katika Utafiti

Nadharia ya umitindo ina mihimili au viwango mbalimbali lakini hatukutumia kila kiwango bali tulitumia tu vile viwango ambayo vinafaa kazi yetu. Viwango ambavyo vilitumika katika utekelezaji kazi hii ni pamoja na:

Ukiushi wa Kilahaja: hiki ndicho kiwango cha nadharia hii ambacho kitatumika kuchambua mtindo wa matumizi ya lahaja tofautitofauti za lugha zinazotumika na msanii. Kiwango hiki kimechaguliwa kwa sababu mwandishi Said Ahmed Mohamed katika riwaya yake ametumia lahaja mbalimbali za lugha ya Kiswahili kama tutakavyo ona hapo mbele.

Kiwango cha kimapisi/ Kihistoria: Hapa kiwango hiki kitatumika kufichua uelementi wa kihstoria katika masimulizi. Mtindo huu unaweza kuja katika namna ambapo mwandishi anawasilisha jambo kwa mara ya kwanza lakini katika mfumo wa kukumbusha yaliyopita katika mandhari ya kazi au jamii iliyobuniwa.

Kiwango cha Kisemantiki: Kiwango hiki kinahusu lugha ya kitamathali na miundo ya lugha ambayo ni sifa muhimu ya kuchunguza matini ya kifasihi tunapotumia nadharia ya Umitindo. Ni jinsi matumizi ya lugha yanavyoathiri maana kwa njia fulani. Ukiushi wa aina hii unahusu matumizi ya maneno na jinsi maana hiyo inavyofasiriwa katika hali za kawaida. Mara nyingi huhusisha matumizi ya maneno 7 kwa njia ambazo si za kawaida kimaana. Huwepo matumizi ya tamathali za usemi: Mbinu za kinaya, kejeli, mbinu ya kweli-kinzani (paradoksi,) sitiari n.k. Pia, huhusisha matumizi ya jazanda, yaani lugha ya picha aidha za kimaelezo au za kiishara (ambazo si taswira au picha tu bali zina ujumbe wa ziada). Maelezo haya ni kulingana na; (Leech na Short 2007:101, Wamitila 2008:518). Viwango hivi vitatu tu ndivyo vilivyo chaguliwa kutokana na upana wake au uwezo wake wa kushughulikia aina mbalimbali za mitindo.

### 2.3.5 Hitimisho

Kipengele cha mapitio ya mandishi kinaonesha kazi mbalimbali katika eneo la mada yangu ambazo nimepitia katika hali ya kujiandaa kushughulikia utafiti huu. Kwa upande mwingine kipengele cha Kiunzi cha nadharia kinajadili na kufafanua mwongozo utakao fuatwa na mfanyaji kazi hii ili kuweza kuleta matokio yanayoafikiana vigezo vya kitaalamu. Sura hii kwa ufupi inatoa ushahidi wa kwamba kazi hii sio ya kibubusa kwana ina jadili kiundalni kazi mbalimbali za watafiti watangulizi ambao kazi zao zimetumika kama msingi wa kiigizo chama cha kufuatwa na utafiti huu

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Hatua hii ya utafiti inajadili na kueleza mapana na marefu ju ya namna ambavyo utafiti huu ulivyofanyika. Sura hii itafafanua namna ambavyo vipengele mbalimbali vya utafiti huu vilivyokusanywa na namna ambavyo vipengele mbalimbali vya utafiti huu vilikusanywa na kuchambuliwa kwa lengo la kufikia matarajio ya utafiti. Sura hii inajumuisha vipengele mbalimbali kama ifuatavyo; mkabala wa utafiti ambao unabainisha mrengo ambao ukusanyaji na uchambuaji wa utafiti umechukua, sampuli na usampulishaji kipengele ambacho hubainisha nyanja ambazo data tafitka zimetolewa, eneo/mipaka ya utafiti kipengele ambacho huonesha kikomo au eneo gani hasa lilizingatiwa na mtafiti, mbinu za kukusanya na kuchambua data; kipengele hubainisha mifumo ilyotumika kukusanya data na kuzichambua, maadili ya utafiti na mwisho kabisa ni muhtsari wa sura nzima.

## 3.2 Mkabala wa Utafiti

Utafiti huu ulifanyika kwa kufuata mrengo wa ubora. Yaani, uchunguzi umefanyika kwa kulinganisha na kulinganua data mbalimbali za utafiti ili kutambua ubora na udhaifu wake kwa ujumla. Ulinganishaji umefanyika sana katika data zilizotolewa katika riwaya ya "UTENGANO" na kazi za wandishi chipukizi ili kubainisha makossa amabayo wanayafanya na mwisho wa siku kushindwa kufikia ubora wa kazi mithili hii ya "UTENGANO". Katika uchambuzi wa data hizi kilichotiliwa umakini ni kutafuta viashiria vya ubora na udhaifu wa data tafitika. Hatua hii inaboresha utafiti kwana inaufanya uwemrahisi kueleweka kwa msomi yeyeto au mhakiki. Hii ni kwa sababu inamsadia msomaji wa kazi hii kuelewa kwa nini mtafiti alichagua data kuzingatia data za aina fulani na kuacha za aina nyingine. Utafiti huu ulitegemea mbinu ya upekuzi wa maktabani.

### 3.3 Usampulishaji

Usampulishaji ni mfumo wa ukusanyaji data ambapo mtafiti huchukua mifano ya data moja au mifano mbalimbali kutoka katika mojawapo ya data tafitika ili kuhakikisha kwamba uchunguzi unafanyika pasi na upendeleo wowote. Katika utafiti huu, riwaya ya "UTENGANO" ndio imetumika kama rejeo la kiada na kwa upande mwingine kazi za wasanii pamoja na wataalamu wengine zikatumika kama marejeo ya kiada. Yaani, usampulishaji mkuu ulifanyikwa kwenye riwaya hii na kazi nyingine za kisanii na kiufundi zikafuatia.

### 3.4 Mbinu za Utafiti

Kila utafiti kulingana na malengo yake hutumia mbinu mahususi kutafuta data na kuchambua data hizo. Yaani, mbinu ya utafiti lazima iendane na malengo ya utafiti pamoja na maswali ya utafiti huo. Hii ni kwa sababu hivi viwili visipopatana huenda mtafiti akakosea mkabala wa utafiti jambo ambalo linaweza kubadili mrengo mzima wa utafiti. Hapo chini mbinu za utafiti huu zitabainishwa kama ifuatavyo;

#### 3.4.1 Upekuzi wa Yaliyomo

Upekuzi ni mbinu ya kuchiunguza na kukusanya data ambayo inatumika kwa namna mbalimbali lakini kwa utafiti huu mbinu hii ilitumiwa kupitia kazi mbalimbali za marejeo ya kiada pamoja na yale ya ziada. Mbinu hii imetumika kwa mwongozo wa malengo pamoja na maswali ya utafiti. Hii ndio mbinu pekee iliyotegemewa katika utafiti huu na ilitumiwa kupitia kazi zifuatazo;

*i.* Riwaya ya *Utengano* (1980)

ii. Ukiushi Kama Elementi Ya Kimtindo Katika Baadhi Ya Riwaya Za Ken Walibora.

iii. Kutathmini Mabadiliko Ya Usawiri Wa Mwanamke Katika Riwaya Ya Utengano Na Kamwe Si Mbali Tena: Utafiti Linganishi

iv. Kichocheo cha fasihi (2003) cha K.W. Wamitila

v. Kamusi ya tashbihi, vitendawili, milio na mishangao (2004) cha K.W. Wamitila.

Kazi hizo hapo zilipitiwa pamoja na nyingine kama zilivyowasilishwa katika kipengelecha marejeo.

### 3.5 Vifaa Na Zana Za Utafiti

Zipo ala au zana mbalimbali ambazo zilitumika katika suala zima la utekelezaji wa utafiti huu. Vifaa hivyo ni kama ifuatavyo;

### 3.5.1 Vitabu

Aina ya kwanzaya vifaa vya utafiti huu ni vitabu. Utafiti huu umetumia Vitabu mbalimbali zikiwemo riwaya kama vile "UTENGANO" kama rejeo la kiada, na nyinginezo kama vile "DUNIA YAO". Lakini pia vitabu vingine vimetumiwaa kama vile Kamusi na hapa hususan ile ya TUKI.

### 3.5.2 Makala Pamoja Na Majarida

Makala mbalimbali za kazi za kitafiti za watafiti watangulizi zimetumika kama zana za kutekelezea utafiti huu na mfano mzuri ni lile jarida la International Academic Journal of Social Sciences and Education | Volume 2, Issue 2, Makala ya Dhana ya Mtindo na Nafasi yake katika Fasihi na vinginevyo kama vilivyowasilishwa katika kipengele cha marejeo.

### 3.5.3 Daftari La Kuchambulia Data Na Kunukuu Mambo Muhimu

Hapa daftari la kubwa vya kutosha lilitumika kama sehemu ya kutengenezea nakala cha na baadae kuhamisha kazi kwenye nakala safi.

## 3.6 Uchanganuzi Data

Mchakato huu kama nilivyotangulia kueleza hapo juu kwenye kipengele 3.5.3, data zilizowasilishwa ziliwekwa kwenye daftari. Kwenye daftari kulinukuliwa kila kitu kilicho dhaniwa kuwa ni muhimu na baadae kupitiwa kwa undani na umakini wa juu. Baada ya hatua hii sasa data zilianza kutenganisha katika zile zilizoufaa utafiti na zile ambazo hazikuufa utafiti. Kisha baada ya hapo kutoka kwenye zilizoufaa utafiti zilitolewa data za utafiti kwa kufuata malengo ya utafiti na maswali yake.

## 3.7 Hitimisho

Kwa kukamilisha kipengele hiki, cha utafiti tutasema kwamba ni wazi kwamba ukusanyanji data na uchambuzi wake ulifanyika kwa ufanisi wa hali ya juu na bila shaka uchunguzi huu hauna hali ya upendeleo wa aina yoyote.

# SURA YA NNE

# MATOKEO YA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii ya utafiti ndio inashughulikia uchambuzi na uchanganuzi halisi wa data za utafiti. Uchanganuzi huu ulifanyika kwa kufuata mwongozo wa malengo na maswali ya utafiti ili kufikia lengo la utafiti. Kabla ya kuingia katika uchanganuzi data za utafiti tuliona kwamba itakua bora iwapo tungeanza na kutoa muhtasari wa riwaya nzima. Hii kwa lengo la kumwezesha msomaji kuilewa kazi inayojadiliwa kupata muktadha wa riwaya nzima japo kwa muhtasari.

Riwaya ya "UTENGANO" imeandikwa mnamo mwaka 1980 na kuchapishwa na Longman.

'UTENGANO' ni riwaya nayoangazia masuala muhimu ya kijamii kama talaka, nafasi ya wanawake katika jamii, taasubi za kiume, siasa, na msamaha.

Upekee wake mkubwa unatokana na jinsi mwandishi Said Ahmedg Mohamed anavyotumia lugha kwa urahisi, lakini kwa jazanda kubwa.

Kazija, mhusika mkuu riwayani ni mpenziwe Bwana Maksuudi, mwanasiasa na mfanyabiashara mwenye ushawishi.

Anapanga njama ya kuwakosanisha Bwana Maksuudi na mwanawe, Mussa.

Anafaulu kwenye mpango huo, pale anapowaita wawili hao kwenye nyumba yake.

Maksuudi na Musa wanapigana vikali, hali inayowafanya kutengana.

Hata hivyo, Kazija anafanya hivyo ili kulipiza kisasi kwa niaba ya mwanawe rafikiye, Biti Sururu. Biti Sururu ni mwanawe Bi Farashuu.

Maksuudi alikuwa amemwoa Biti Sururu, ambapo alimdhulumu na kumtaliki. Kutokana na masaibu hayo, Biti Farashuu anageuka kuwa maskini, anajiingiza katika ulevi na kufariki baadaye.

Mwandishi anawatumia wahusika Shoka na James kuonyesha jinsi watu maskini katika jamii wanavyofanya kazi kwa bidii kutafuta riziki. Hata hivyo, badala ya kutumia mapato yao kujiendeleza kimaisha, wanajiingiza katika ulevi na kuzitelekeza familia zao.

Nao Bwana Maksuudi na Bwana Smith wanasawiriwa kuwa watu walaghai katika jamii wanaoipora serikali. Riwaya hii inaangazia kwa undani, nafasi ya mwanamke katika jamii. Mfano huu unadhihirika kwenye maisha anayopitia Bi Tamima, mkewe Bwana Maksuudi.

Ni mwanamke aliyedhulumiwa sana. Amezuiwa kuifahamu dunia na kufanywa mtumwa bila yeye kutoa sauti yoyote.

Mumewe anaenda nje ya ndoa bila kumheshimu hata kidogo.

Maksuudi anamtaliki baada ya kumpiga siku moja baada ya kujifungua, sababu kuu ikiwa hatua yake kumkubalia mkunga kuingia nyumbani mwake. Suala jingine linalojitokeza riwayani ni mtindo wa baadhi ya wanawake kuwaharibia maisha wenzao kimakusudi, bila kujali athari za vitendo vyao. Kwa mfano, Mama Jeni anauza pombe ambapo pia anamiliki danguro.

Ana wanawake ambao wanashiriki biashara ya ngono, wanaowahadaa wanaume na wasichana wadogo kushiriki kwenye ukahaba.

Maimuna, ambaye ndiye mhusika mkuu riwayani, anapevuka sana kutoka hatua moja ya maisha hadi nyingine. Alikuwa msichana aliyefungiwa kwao, lakini anatoroka na kuishia kufanya kazi kazi katika danguro la Mama Jeni.

Baada ya mkondo wa maisha yake kuharibika, anakubali kwamba hahitaji kitu chochote kizuri maishani. Anaelekea katika kijiji pweke cha Futoni, kilicho karibu na ziwa. Licha maisha yake mabaya, anakutana na mwanamume aitwaye Kabi, ambaye anamwoa licha ya matatizo yaliyokuwepo awali. Ndoa yao inajenga daraja la msamaha kati ya Bi Farashuu, Mussa na Maksuudi.

Ni riwaya inayoonyesha kuwa licha ya vitendo vyetu kama binadamu, kila mmoja anahitaji msamaha na Mungu ndiye mwenye uwezo wa kumhukumu mwanadamu.

### 4.2 Mitindo ya Uwasilishaji Ujumbe wa Kazi za Utanzu wa Riwaya.

Fasihi kama sana ya lugha inatumia njia mbalimbali za uwasilishaji. Njia hizi hutokana na ubunifu au utashi wa mwandishi. Yaani, hakuna njia thabiti zinazojulikana au zilizowekwa hususan kwa lengo hili na hivyo basi uamuzi wa njia mwafaka kwa ajili ya kuwasilisha ujumbe wowote wa kifasihi hutokana na matakwa au maoni ya mwandishi. Njia hizi za uwasilishaji ndio hutambuliwa kwa istilahi ya (mi)mtindo. Uanishaji wa mitindo hii ya uwasilishaji ni kama ifuatavyo;

#### 4.2.1 Aina za Mitindo ya Uwasilishaji wa Kazi za Fasihi

Kabla ya kuingia katika uainishaji wa mitindo tuanze na kufafanua upya dhana ya mtindo;

Kwa mujibu wa Senkoro (1982) anasema mtindo katika kazi ya fasihi ni ile namna ambayo msanii hutunga kazi hiyo na kuipa sura ambayo kifani na kimaudhui huainisha kanuni au kawaida zilizofuatwa (za kimapokeo) ama ni za kipekee. Anaendelea kusema, mtindo ni

upangaji wa fani na maudhui katika kazi ya fasihi kwa njia ambayo hutokeza au huonyesha nafsi na labda upekee wa mtungaji wa kazi hiyo.

Wamitlia naye (2003) naye anasema ‘mtindo ni jumla ya mbinu au sifa zinazomwezesha mwandishi kuwasilisha ujumbe wake, huelezea mwandishi anavyounda kazi yake’. Anaendelea kusema, dhana ya mtindo hurejelea sifa maalumu za mwandishi au mazoea ya mwandishi fulani ambayo hujionyesha kwenye fani yake, mazoea hayo ya mwandishi ya kuandika, kuteua msamiati, tamathali za semi, taswira, uakifishi, sentensi na kadhalika ndio yanayompambanua mwandishi huyu na mwanzake.

Kitu anachokisema hapa Wamitila hakitofautiani na Senkoro, kinachoongelewa hapa ni upekee wa mwandishi husika lakini Wamitila kasema kitu kimoja zaidi, kwamba msanii anaonekana kuwa na mtindo fulani kwa sababu amezoea kutunga kazi zake za fasihi kwa namna fulani ambayo inadhihirisha upekee wake. Kwa kauli hii ya Wamitila tunaweza kusema kwamba mtindo wa mtunzi huonekana baada ya kuandika kazi zake kadhaa na kimsingi hii ndio huleta maana halisi ya mazoea. Nakubaliana na kauli hii, kwani hata hivyo huwezi ukahitimisha kuwa mtunzi fulani mtindo wake ni huu kama umesoma kazi yake moja tu, kwa hiyo mtindo (upekee) wa mwandishi huweza kubainishwa baada ya kupitia kazi zake kadhaa na ndipo tunaweza kuona mazoea ya mwandishi huyo katika kuandika kazi zake.

Kwa sentensi fupi tunaweza kusema kuwa mtindo ni ule upekee alionao mtunzi wa kazi ya fasihi katika kuipa kazi yake sura fulani kifani na kimaudhui ambapo mtunzi mwingine hawezi kufanya hivyo hata kama kitu kinachoongelewa ni kilekile.

Sasa mtu anaweza kujiuliza, nitawezaje kubainisha mtindo wa mtunzi katika kazi ya fasihi? Swali hili linaweza kujibiwa kwa kuangalia vipengele fulanifulani.

Tunapotaka kujua mtindo wa msanii katika kazi husika, kwa mfano katika riwaya tunaangalia vipengele vifuatavyo:

### 4.2.2 Matumizi ya Lugha

Hii ni njia mojawapo ya uwasilishaji wa ujumbe itumiwayo na wandishi mbalimbali wa kazi za kifasihi na riwaya zikiwemo vilevile. Hapa tunaangalia aina ya lugha aitumiayo mwandishi wa kazi ya fasihi. Hivyo basi, tutajiuliza maswali yafuatay; Je, mwandishi ametumia lugha ngumu au lugha ya kiufundi? Au mwandishi ametumia lugha ya kinusu ufundi au lugha ambayo ni wastani (yaani, kazi yake ni rahisi kueleweka pamoja na kuwa haijatumia sana msamiati wa kkawaida). Mtindo huu unabainika kupitia msamiati alioutumia mwandishi. Kazi za kiufundi huwa na msamiati mgumu sana na ambao hautumiki sana katika maisha ya watu ya kila siku bali hurejelewa sana katika mazingira au nyanja za wasomi. Kazi za kinusu ufundi

huwa na msamiati ambao unafaa mada za kiusomi na maisha ya kawaida ya watu na zile za kawaida huwa na msamiati ambao ni mrahisi sana kueleweka na kwa mara nnyingi hadhir ya kazi hizi huwa ni wasomi wa daraja ya chini kabisi mfano shule za msingi. Kikubwa cha kuzingatia ni kwamba ifikapo katika kazi za kifasihi pia tunazingatia matumizi ya mbinu nyingine za lugha kama vile tamathali za usemi yaani, tashbiha, tashihisi, na vinginevyo.

Katika uchambuzi iligundulika kwamba mwandishi wa riwaya hii ametumia lugha ya kati na kati. Yaani, ametumia msamiati wa kifundi katika riwaya yake akiuambatanisha mbinu za matumizi ya lugha lakini wakati huohuo akijaribu kuyarejesha mazungumzo ya wahusika wake katika hali ya maisha ya watu ya kila siku jambo amabalo huongeza hali ya mvuto kwa msomaji wa kazi ya mwandishi. Ushahidi wa jambo hili ni wingi wa matumizi ya misimu katika kuwasilisha mazungumzo ya wahusika wake. Mifano kutoka kwenye riwaya:

i. Mbinu ya mdokezo. Hii ni mbinu ya matumizi ya lugha ambapo mtunzi wa kazi ya fasihi hutumia alama ya kituo ambayo mara nnyingi hudokezwa mara tatu. Mbinu hii hutumika kumfanya msomi wa kazi ya imma kutafakari kwa kina juu ya kazi husika au wakati mwingine mbinu hii hutumika kuonesha kwamba mhusika mzungumzaji anasita wakati anaposema maneno yanayojadiliwa. Kwa mfano katika kitabu mwandishi, ‘Sijui tena imekuwaje, lakini mimi nilipomkuta alinambia …’. Pia kwenye ukurasa wa 124, ‘Mradi…m... mradi matatizo...’. Isitoshe pia katika sura ya kumi na mbili ukurasa wa 150, ‘Haya lenda, kama hakuja…’

ii. Matumizi ya lugha ya misimu. Misimu ni vilugha ambavyo hutumika na wazungumzaji wa lugha fulani hasa vijana na ambayo hutumika katika muda fulani na kisha baadae kutoweka. Mfano mzuri katika riwaya hii kwenye sura ya kumi mwandishi anasema kwamba, “SHOKA alikuwa barubaru mmoja, fahali wa mtu, kavundumka mwili na kakacha misuli.” Maneno kama vile, ‘kuvundumka, kukacha na barubaru na kadhalika maneo haya sio Kiswahili sanifu bali huzaliwa katika kipindi fulani cha kisiasa na kisha kutoweka baadae.

iii. Mbinu ya majazi. Mbinu ya majazi ni mbinu ya matumizi ya lugha ambapo mwandishi humpa mhusika jina ambalo huendana au huakisi tabia/mienendo au sifa zake. Aidha majazi inaweza kuwa mbinu ya Sanaa.

Majazi ni mbinu ya mhusika hupewa jina lake rasmi (jina la kuzaliwa) linaloambatana na tabia/mienendo/sifa zake. Aidha, majazi inaweza kuwa mbinu ya sanaa. Mhusika Bahati katika riwaya; ikiwa maisha yake yatadhihirisha kuwa na bahati nyingi; basi hiyo itakuwa ni mbinu ya Majazi.

Mzee Tumbo Kubwa anapenda kula sana kana kwamba hashibi.

Neema ni msichana mzuri, mpole, mpenda amani

Katika riwaya hii mbinu hii imetumika sana lakini mfano Dhahiri kabisa ni ule wa jina la kitabu la ‘UTENGANO’ Mtunzi amekipa kitabu chake jina ambalo huakisi yaliyomo. Tunaona utengano aina mbalimbali za utengano katika riwaya nzima yaani, upo utengano wa wazazi na watoto au wanawao kama vile Bwana Makusudi na wanawe Mussa na Maimuna. Pia tunaona utengano baina ya bwana Makusudi na wakeze kama vile Tamima na Farashuu.

### 4.2.3 Mtindo Wa Dayalojia

Matumzi ya dayalojia. Dayalojia kwa lugha ya kawaida tunaweza kusema kwamaba ni majibizano ya kimazungumzo mtunzi anawasilisha ujumbe wake kwa kuweka mazungumzo baina ya wahusika wawili. Hii ni mojawapo ya mbinu ambazo hutumika Zaidi na watunzi wa kazi za kifasihi. Pia mbinu hii ina utanzu mzima ambao kwa asilimia kubwa huitegemea. Katika riwaya hii tunaona kwamba mbinu hii tukitathmini vizuri uwezekano mkubwa wa kwamba itaibuka katika nafasi ya pili kutumiwa na mwandishi.

i. Mtindo huu umetumika katika riwaya hii kama ifuatavyo;

Biti Kocho aligonga mlango. Mara ya kwanza, kimya. Mara ya pili, kimya. Mara ya tatu ndipo sauti ya Farashu ilipozuka.

‘Nani?’
‘Miye bibi we.’
‘Wewe nani?’
‘Mimi Kocho.’
‘He, Kocho hizo mbona saa hizi?’
‘Ee bibi we, hebu fungua.’
‘Haya dada.’
Baada ya muda mfupi… mwisho wa kunukuu.
*Utengano* (1980, uk….)

#### 4.2.4 Mtindo Wa Barua

Hii ni njia ya uwasilishaji wa ujumbe wa kazi ya kifasihi amababo mtunzi huwasilisha ujumbe wa kipengele fulani cha kazi ya fasihi kwa kutumia mhusika mmoja kumwandikia barua mhusika mwingine. Hapa mtunzi anajenga kazi yake kwa kuhadithia kwa mfumo wa barua kusomwa na mhusika mwingine. Mtindo huu unaingiza hali ya mguso wa uhalisia kupitia kutolewa kwenye masimulizi ya mfululizo kujenga hali ya uandishi na usomaji barua hiyo na mtu mwingine. Mtindo huu umetumika katika barua hii kama ilivyo katika kazi nyingine za mwandishi huyu Said Ahmed Mohamed.

Kwa mfano kwenye sura ya tisa (uk.108) tunaona barua ya Bi Tamima kwa bwana Makusudi kama ifuatavyo;

> "Mintarafu ya barua zako tano nilizozipata mud ahata muda. Sikuweza kukujibu kwani sikuwa na la kunena na la kukutosha muungwana kama wewe. Leo nimeona nijaribu, baada ya kuwaza kauli ya kunena. Lipi tena unalolitaka kwangu? Ikiwa mapenzi umeyasagasaga. Mwanangu mchanga umemuua na wawili sijui umewaeleza wapi. Pamebakia nini baina yetu? Labda roho yangu ambayo nusra uitowe. Na sasa siko tayari kukupa. Sirudi. Tamima.".

#### 4.2.5 Mtindo wa Nyimbo au Ushairi.

Hii ni njia uwasilishaji wa ujumbe katika kazi ya Fasihi ambapo mwandishi huwasilisha maudhui miongoni mwa nyingine katika kazi yake kwa mtindo wa kutumia mashairi au mziki. Mtindo huu unakuza hadhi ya kazi ya fasihi na huonesha ufundi wa mwandishi. Mtindo huu pia umetumika sana katika riwaya hii kama tutakavyoonesha hapo chini;

Katika sura ya kumi ukurasa wa 125 "…Muziki ulipofika pahala fulani, alianza kuimba,

> "Nina kovu, nina kovu, wanitonesha kwa inda,
> Ukikatazwa maovu, Warudi wenda yatenda?
> Wanitia roho mbovu, Kwa sababu nakupenda?
> Nakupenda, nakupenda, Kwa sababu nakupenda.
>
> Hapo aliitikiwa na wenzake. Tena muziki ukampokea kwa matao yaleyale, na tena wakati ulipowadia, aliingia katika mizani yake.
>
> "Kama hunitaki nena, Usende nami kwa hila,

La kwanza si maungwana, Na la pili sio mila,
Jambo la kudanganyana, Ni jambo lenye madhila,
La madhila, la madhila, Ni jambo lenye madhila
Mfano mwingine ni ule wa shairi la Inspekta Rashid."

Mfano mwingine ni katika sura ya sita ukurasa 71;

"Akakumbukia ubeti wa shairi lake alilotunga karibuni katika jumla ya mashairi anayokusanya katika kitabu atakachokiita Kilio cha Wanyonge, alianza:

"Nyuma kule wanakotoka,
Wanyonge hawa wanyonge,
Walilima, lakini mavuno,
Hawakuyaona, hawakuyaona,
Na Wafanyakazi,
Wafanya kazi, walimenyeka,
Lakini walilala na njaa…
Njaa, ndiyo ilikuwa misumeno
Iliyokeketa matumbo yao,
Na maradhi, yalikuwa nduli wao,
Na ujinga ulikuwa kiza chao…
Shibe, uzima, matibabu na elimu
Walipewa mabwana wao…
Na sasa, matarajio ya uhuru,
Wapi shibe? Wapi uzima Wapi elimu?
Nasikia,
Nasikia nduli…Naona adui bado,
Bado Afrika inatawaliwa,
Inatawaliwa kwa mlango wa nyuma…
Utawala mamboleo,
Wa nje kule utokeako,
Na ndani uendelezwako…"

### 4.2.6 Mtindo wa Ukuzaji wa Wahusika.

Ujenzi wa wahusika siyokipengele tu cha kazi ya fasihi bali ni mbinu ya uwasilishaji wa ujumbe wa kifasihi. Hii ni kwa sababu kila Hali au tabia ambayo anadhihirishwa nayo mhusika fualani husaidia kubeba maudhui fulani ambayo mwandishi anataka kuwasilishwa. Katika riwaya hii imetumia wahusika mbalimbali na tunaweza kusema kwamba aina kuu ya wahusika ambayo imetumika katika riwaya hii ni wahusika mviringo. Wahusika wake amewagawanya katika vikundi mbalimbali wakiwa katika makundi makuu matatu yaani, wahusika wanawake na wanaume, watoto pamoja na watu wa kawaida au wafanyakazi.

i. Wahusika Wanawake

Mwandishi amegawanya wahusika wanawake katika makundi mawili wanaonyanyaswa na wanawake wakombozi. Katika wanawake mwandishi ametumia wahusika kama vile Bi Tamima, Bi Farashuu, Kazija, Maimuna, Bi Kocho na wenginewo. Hawa wametumiwa kujenga maudhui ya ukombozi wa mwanamke kutoka katika unyanyasaji wa taasisi za kidini na kiutamaduni. Hapa mwandishi anatuonesha namna wanawake hawa wanavyonyimwa haki zao za msingi kama vile uhuru wa kutembea na kuekwa kwenye utawa majumbani mwa watu kama vile bwana Makusud. Pia tunaona mateso mbalimbali ambayo wanawake hupitia majumbani humo. Mifano ya wahusika wananwake ambao ametumia mwandishi ni pamoja na Bi Tamima, Bi Farashu, Maimuna. Maudhui hii inaakisi uhalisia wa maisha ya jamii nnyingi katika dunia ya leo.

Kwenye upande wa wanawake wakombozi mwandishi ametumia wahusika wanawake kama vile Kazija ambaye ananuia kulipiza kisasa kwa ajili ya mabaya ambayo anatendewa rafikiye Farashuu wakati anapokuwa bado mke wake bwana Makusudi. Pia mwanamke mwingine ambaye anakuja kwenye sura ya ushujaa na ukombozi ni Bi Kocho ambaye anampinga vikali Makusudi na kumkomboa Bi Tamima kutoka katika ndoa iliyojaa unyanyasaji.

Pia mwandishi amechorwa upande mwingine wa wanawake kama vile mama Jeni ambaye anafanya biashara uuzaji Malaya jambo ambalo linachangia vikali uangamizaji wa maisha ya wanawake. Pia katika jamii zetu leo tunaona kwamba taswira za wanawake hawa zipo.

Ukuzai wa wahusika katika wahusika wa kike unaonekana katia riwaya kupitia hali ya kwamba wanabadilika kutoka hali ya unyonge na mateo na kubadilika kuwa watu jairi ambao wapo tayari kupiania haki zao na kukabili ugumu wowote wa maisha. Hali hii inadhihirishwa kupitia barua ya Bi Tamima mathalan ambaye hatimaye anapata uwezo wa kumibu mbaya wake Bwana Makusuudi.

ii. Wahusika Wanaume

Wahusika wanaume wa riwaya hii tofauti na wale wa kike mwandishi amewalrta katika sura tofauti-tofauti. Wapo ambao mwandishi amewachora kama watu wasimamizi wa haki na wapigania wanyonge kama vile Rashid ndugu yake Bwana Makusudi. Mwandishi amemleta kama mtumishi wa jeshi la polisi ambaye yupo kwenye daraja la uinspekta. Wahusika kama Fadhili ni wache wache sana ambao wanao moyo wa kuhurumia wanyonge na kupigania haki zao. Taswira hii ya mwandishi inaakisi ilivyo maisha halisi ya jamii za waswahili wengi na nyinginezo. Jamii nnyingi katika dunia ya leo zimepatwa na maradhi ya ubinafsi na uchoyo. Yaani, ni mfumo wa kila mtu kupambana na hali yake. Mfumo kunusurika kwa wenyeuwezo na kuteketezwa kwa wanyonge.

Kwa upande mwingine amemjenga mhusika bwana Makusudi kama mtu ambaye alianza maisha akiwa mtu wa kutetea haki za wanyonge na miongoni mwa mashujaa waliwo jitahidi kuona kwamba taifa lao linapata uhuru. Lakini mara baada ya kufanikiwa kumtoa mkoloni, Makusudi alibadilika na kuanza kuwatendea Wafrika wenzake vile walivyokuwa wakitendewa na Wakoloni. Jambo hili linaakisi uhalisia wa mataifa mengi ya Afrika mara tu baada ya kuapata ukoloni. Hii ndio sababu kubwa nyuma ya wandishi mbalimbali kuandika kazi kama vile 'THINS FALL APART' cha mwandishi CHINUA ACHEBE, au hata ile tamthilia ya mwandishi FRANCIS IMBUGA ya 'BETRAYAL IN THE CITY'. Dhamira kuu ya kazi hizi zote ilikua ni kufichua maovu ya viongozi wasaliti wa mataifa machanga ya Afrika na kupiga vita uongozi mbaya.

### 4.2.7 Namna ya Usimulizi

Katika namna ya uwasilishajitunachozingatia ni mfumo ambao mwandishi anatumia kuwasilisha kazi yake. Katika huu mtindo wa uwasilishaji ujumbe swli la muhimu kujiuliza ni, "Je, mwandishi ametumia nafsi gani kuleta ujumbe wake kwa hadhira lengwa. Yaani, ni nafsi ya kwanza, ya pili au ya tatu.

Nafsi ya kwanza ni mfumo wa uwasilishaji ujumbe ambao mwandishi wa kazi ya fasihi hutumia mhusika mkuu au mhusika mwengine yeyote kusimulia hadithi akiwa yeye ndio mtenda au mtendewa. Yaani, katika fumo huu mhusika anasimulia yanayomsibu binafsi. Nafsi ya pili ni mfumo wa usimulizi ambao mwandishi husimilia hadithi kwa kutumia mhusika mmoja kunena kwa hadhira yaliyomsibu mhusika mwengine. Katika nafsi ya tatu mwandishi ndio mjuzi wa kila jambo na ndio msimulizi mkuu wa visa na matokeo yote ya kazi husika. Nafsi ya tatu hutumiwa na mwandishi kutuelezea kazi yake moja kwa moja passi na kutegemea

mhusika yeyote kama chombo mbadala. Said Ahmed Mohamed katika riwaya hii ametegemea sana mfumo wa masimulizi wa matumizi ya Nafsi ya kwanza. Nafsi ya kwanza na ya pili zimetumika sana pale ambapo mtindo wa dayalijia umetumika. Yaani, zimetumika kutoa maelezo katika mtindo wa dayalojia.

Mifano ya kutoa ili kudhihrisha mtindo huu katika riwaya hii ni mingi mno lakini tutatumia jambo rahisi Zaidi kama mfano. Ukititazama ufunguzi wa kila sura ya kitabu hiki utagundua ya kwamba sura hizi zinaanza kwa nafsi ya tatu.

#### 4.2.8 Ubadilishaji Wa Hati Au Mfumo Wa Herufi

Katika njia hii ya uwasilishaji wa ujumbe, mwandishi wa kazi ya fasihi mwandishi hubadili mfumo wa uandishi wa herufi ili kuleta upekee wa maudhui au kutofautisha aina moja ya maudhui kutoka nyingine. Katika riwaya hii, mwandishi ametumia sana mfumo wa kawaida kwa herufi za 'Times New Roman'. Mifumo mingine ya kiherufi imetumika katika baadhi ya sehemu kama vile;

Katika sura ya kumi na moja mwandishi Said Ahmed Mohamed anafungua sura kwa kusema, "BWANA MAKUSUDI alilazwa hospitali. Pia katika sura ya kumi ukurasa wa 116 mwandishi anasema, "MOONO, PONDS, podari ya HIMALAYA, SNOW na kadhalika. Unapokosa uzuri wa kimwetu, utafanyaje? Hiyo ndiyo siasa ya Maimuna. Pamoja na hayo, vichupa vya mafuta mazuri, vyengine vya mkokoriko, na vyengine vya mafuta ya kujipaka, kama KAMA LADY GAY, PEACE OF HEAVENS, HYPNOTIC…

Mtindo huu unatumika kwa lengo la kuvuta umakini wa watu kwenye jambo fulani, kuepusha msomaji kuchanganya majina ya vitu maalum na maneno ya usimulizi, kumwezesha msomaji kujenga picha ya uhalisia katika kichwa chake.

Mwandishi wa kazi hii ametumia mbinu nyingi ila katika utafiti huu tumetumia tu baadhi ya mbinu.

### 4.3 Namna ya Kutumia Mitindo ya Uwasilishaji wa Kazi

Hakuna namna mahususi ya kutumia njia au mitindo ya kuwasilishia ujumbe katika kazi ya kifasihi. Hii ni kwa sababu fasihi ni kazi ya kubuni ambayo hutegemea ubunifu au utashi wa mwandishi. Katika kila utanzu wa fasihi zipo baadhi ya kanuni ambazo hutumika ila kanuni hizi ni kwa ajili ya kutoa tu mwongozo na sio kuelekeza hatua kwa hatua namna ambavyo kazi nzima inapaswa kufanyika. Katika kazi ya Sanaa yoyote uhuru wa mtunzi ni jambo muhimu. Hii ni sababu ya utokeaji wa mgogoro wa fasihi katika wanaushairi.

Kwa maelezo hayo, ili mtu aweze kutumia vyema mitindo hii hana budi kuzingatia baadhi ya ili kuepukana na baadhi ya mambo. Mambo hayo ni kama ifuatavyo:

### 4.3.1 Uchaguzi wa Mada.

Kazi yoyote ile haiwezi kuendelea bila ya mada iwe mbele ya hadhira au wakati wa kuitengeneza kazi hiyo msanii. Hii ni kwa sababu mada ni kipengele, muhimu sana cha kazi ya fasihi. Mada hubeba muhtasari wa kazi au kwa namna nyingine tunaweza kusema mada ndio sura ya kazi. Bila ya kuwa na mad hata ule mtiririko wa mawazo ya kutengenezea kazi utapotea jambo ambalo linaweza kupelekea kukosea kuchagua mtindo mwafaka kwa ajili ya kuwasilishia ujumbe fulani. Hii ni kwa sababu wazo huongoza uchaguzi wa mtindo na wala sio mtindo kuongoza uchaguzi wa mawazo.

### 4.3.2 Kusoma na Kuelewa Mada

Hata kama kazi za fasihi huwa ni za kubuni lakini mandalizi jambo lisiloepukika katika utunzi wa aina yeyote ile. Hii ni kwa sababu uoga utokanao na ujinga ni miongoni mwa vyanzo vikuu vya kuzuia watu kutumia utasshi wao au uhuru. Hii ni kwa sababuunamfanya mtu kukosa kule kujiamini na kudhani mara kwa mara kwamba anakosea kila anapojaribu kujieleza. Hivyo basi, ni muhimu sana kujianda ili kujihamii na maarifa stahiki kwa kazi husika ili kuepuka vikwazo vya kioga.

### 4.3.3 Kuoanisha Mandhari na Toni

Mandhari ni ni sehemu ya kufikirika inayotengenezwa na mwandishi wa kazi ya fasihi kama sehemu ambapo visa na matokeo hufanyika. mandhari inaweza kuwa ya kijijini, mjini, vitani, garini, msituni na kadhalika. Kwenye upande wa toni, tunaweza kusema kwamba toni ni sura kazi ya fasihi inayodhihirika akilini na sio katika uhalisia. Toni ni ilehisia au ufahamu unaoingia akilini mwa hadhira baada ya kusoma kazi fulani. Ni juu ya kila mwandishi kuhakikisha kwamba kuna uwiano baina ya mandhari ya kazi na toni. Haiwezikani kuzungumzia juu ya maisha ya kimasikini ya watu wa jamii fulani katika kazi wakati tunaona wahusika wako wakiwa na taswira za unene. Kusimulia juu ya sehemu ya kitajiri wakati ukitumia wahusika ambao wamevaa nguo za hovyo au barabara ziwe zenye mashimo na kadhalika.

### 4.4.0 Makosa ya Utunzi wa Riwaya

Hakuna msanii mwenye kazi iliyokamilika mia kwa mia. Yaani, kazi yoyote ile lazima iwe na mapungufu kwa namna moja au nyingine hata yawe madogo kiasi gani. Hii ni kwa sababu hakuna ambaye hakosei sharti awe ni kiumbe hai. Hii haina maana kwamba tujivunie kukosea bali tunatakiwa kujifunza kutokana na makosa tuliyotanguliza au makossa ya watu wengine. Kipengele hiki cha utafiti kitajaribu kuonesha namna watu mbalimbali wanavyokosea katika utumiaji wa mitindo ya uwasilishaji wa kazi ya kifasihi. Ni muhimu sana watu kutambua utelezi unaojitokeza katika utumiaji wa mitindo ya uwasilishaji wa kazi za kifasihi. Hii sio kwa sababu tu ya kuepuka kurudia makosa yale yale bali inasaidia kukuza kiwango cha ubora wa kazi zinazotolewa katika utanzu wa riwaya na hivyo basi kukuza fasihi kwa ujumla. Makosa mengi tutakayo jadili hapa wandishi hufanywa na wandishi chipukizi amba Makosa ambayo hufanyika katika kutumia mitindo mbalimbali ya uwasilishaji wa kazi za fasihi ni pamoja na;

### 4.4.1 Unganganizi wa Mtindo Mmoja

Baadhi ya wandishi wanapoandika kazi riwaya za hungangania sana mtindo mmoja. Hapa jambo hili linadhihirika sana katika mtindo wa masimulizi. Unakuta kwamba mwandishi anatumia lugha ya kinathari kupita kiasi na mwisho wa siku kutupa mitindo mingine pembeni ambayo inge nogesha kazi yake na kuipa ile ladha ya kiufundi. Ili mtu aweze kutumia mitindo vizuri lazima awe mwepesi wa kuoaisha mtindo stahiki pale inapobidi. Hii ni kwa sababu mtindo kutumika kuwasilisha ujumbe maana yake hutumika kuwasilisha maudhui katika muktadha fulani. Yaani, katika muktadha ambapo kuna masafa marefu baina ya wahusika utakuta mwandishi anajenga mawasiliano baina yao kwa kutumia mtindo wa simu au uandishi wa barua. Tatizo kubwa ambalo huibuka kutokana na unganganizi wa mtindo mmoja ni kwamba inafika wakati ambapo hadhira itakereka urudiaji wa kitu komja. Mfano tukiangalia namna ambavyo mbinu ya ubadilishaji wa hati au mfumo wa mandishi imetumika, unaona kwamba mwandishi ameitumia kwa usawa. Laiti mwandishi angelikuwa amekithiri sana kubadilisha mifumo ya mandhishi, kazi yake ingekuwa inachosha kusoma na huenda ingekera baadhi ya wasomi.

### 4.4.2 Waandishi Chipukizi Kuigaiga

Msisimko wa kazi yoyote ya kifasihi hutokana na mwandishi kutunga kazi ambayo inatokana na ubunifu wake na kuiwasilisha kwa namna ambayo inampwekesha au inamtenga na watunzi wengine. Kukosekana kwa mguso huu katika kazi inasababisha kazi kuwa ya kawaida sana na hata kukosekana kwa wasomi au hadhira. Hii ndio sababu wengi kati ya wandishi chipukizi

hawatambuliki na watu hadi wanapoanza kujiamini kutoa kazi pasi na kuangalia kazi za wabobezi wa tanzu za fasihi husika.

### 4.4.3 Matumizi ya Lugha

Katika mtindo huu wapo baadhi ya wandishi ambao hawatilii sana umuhimu katika suala zima la matumizi ya mbinu za lugha na hivyo kufeli kuafika kipengele au mtindo huu. Matumizi ya lugha ndio huipa kazi ya kifasihi ladha ya kiubunifu ndio maana tunawza kusema kwamba kazi bila ya mbinu za lugha ni sawa mboga bila ya viungo. Ubunifu sio mwendo wa kubuni tu visa na matokeo bali mchakato mzima hupata ladha yake kupitia uwezo wa mwandishi kucheza na lugha ili hadi kutoa kazi yenye mvuto. Tunachoita kazi kuwa yenye kusisimua ni ule uwezo wake kumfanya msomii kushangaa juu ya namna mwandishi anavyomudu matumizi ya lugh. Uwezo wa mtu kutumia lugha katika namna ambayo inamtofautisha na wanajamii wenzake wote na hivyo basi kudhirisha ufundi wa kazi yake.

### 4.4.4 Kutofahamu Hadhira

Ni muhimu kuchagua mtindo unaofaa kwa hadhira yako. Kwa mfano, kutumia lugha rasmi kwa watoto au lugha isiyo rasmi kwa wasomi inaweza kusababisha kutokuelewana. Hivyo basi kila mwandishi anapotunga kazi yake hanabudi kutathmini hadhira lengwa na kubaini uwezo wao na kiwango chao cha eimu na maarifa ili aweze kuwaletea kitu ambacho hakitowakatisha tamaa. Maana watu weni hukata tamaa na wakati mwingine huchukia mambo ambayo huwapa wakati mgumu kueewa au kusoma.

### 4.4.5 Kutumia Maneno Yasiyo Sahihi

Hii inatokea mara nyingi katika jitihada za wandishi za kupwekesha kazi zao na kutaka zionekane ni za kiuundi Zaidi kuliko kawaida. Maneno yanayochaguliwa yanapaswa kuwa sahihi na kueleweka kwa urahisi. Kutumia maneno magumu au yasiyo ya kawaida kunaweza kufanya maandishi yako kuwa magumu kueleweka. Jambo hili pia linaweza kutokana na kutotaiti mada yako ya utunzi ipasavyi na mwisho wa siku kufeli katika uchaguzi wa mada. Mwandishi yeyote anapaswa kuchunguza mada yake kwa kina ili kubaini msamiati mwafaka kwa maudhui mbalimbalai alizo nazi. Pia mwandishi hanabudi kuthibitisha ya kwamba msamiati anaotumia hata kama ni kwa njia ya ubunifu una asili katika lugha husika.

### 4.4.6 Utumiaji Lugha Ya Matusi

Qadhia ya uandishi ni ya kiungwana na waa sio suala la vijiweni na hivyo basi kutumia lugha ya hovyo kunaweza kuwakera wasomaji au hadhira yako na kupunguza uaminifu wako. Pia

fasi inatambulika kama kioo cha jamii na haiwezikani kioo jamii kuwa ni chenye dhamana ya usambazaji mmomonyoko wa maadili. Yaani, jamii na fasihi ni mambo mawili yanoyoathiriana na hivyo basi zikianza kutolewa kazi zilizokithiri lugha ya matusi basi punde si punde tutaona mabadiliko hasi katika tabia za wanajamii. Hivi leo sio ajabu kuona kwamba kukua kwa wimbi la utunzi wa riwaya pendwa na tamthilia za mrengo huo kumezua tatizo vijana kuingia kwenye habari za mapenzi wakiwa wadogo sana kiumri.

### 4.4.7 Kutumia Mitindo Iliyopitwa Na Wakati

Mwandishi yeyote ili kazi zake ziendelee kudumu na kupata umakini wa watu hanabudi kujitahidi kuenda na mabadiliko ya watu. Mfano mzuri tukimtizama Said Ahmed Mohamed ambaye alianza kuandika katika miaka ya nyuma tunaona kwamba alirejelea sana matumizi ya barua katika kazi zake. Katika kazi ya UTENGANO alitumia mtindo huu kupitia mhusika Bi Tamima na Bwana Makusudi na pia katika riwaya ya DUNIA YAO anatumia mtindo huu kupitia mhusika Mtima wakati akimwandikia baba yake. Hii katika wakati wake ulikuwa mtindo wa aafu kabisa. Lakini katika dunia ya leo ambayo imeingia katika utandawazi mwandishi hanabudi kuakisi mitindo hii katika kazi zake. Ndio maana tunaona kwamba hata mwandishi Said Ahmed Mohamed analigusa suala la utandawazi hata kama sio moja kwa moja kupitia maneno ya baba yake Mtima baada ya kupokea zawadi ya laptop kutoka kwa binti ye.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Mtindo kama kipengele cha fasihi kimejadiliwa sana hapo kabla na wataalamu wa fasihi kama tulivyo tangulia kuonesha, ila katika sura hii tutajaribu kuhitimisha uchunguzi wetu kwa kugusia juu ya baadhi ya nukta kuu na kutoa mapendekezo machache yanayoendana na kazi hii. Sura hii itahusisha vipengele vifuatavyo; yaani, itaanza na muhtasari wa kazi nzima kisha, tutaingia kwenye kipengele cha mapendekezo ambacho tutakigawanya katika sehemu mbili na kisha hitimisho la sura.

## 5.2 Muhtasari wa Utafiti

Mada ya mtindo imetafitiwa na wataalamu wengi watangulizi ambao wameigusia katika njia mbalimbali. Lakini pamoja na kazi zote zilizowahi kuwasilishwa chini ya mada hii, ilikuwa bado kupatikana kazi ambayo inaangazia juu ya matumizi ya mitindo katika utanzu wa riwaya. Utafiti huu ulifanikiwa kujadili aina mbalimbali za mitindo inayotumika katika uandishi au utunzi wa riwaya na kisha kutoa mifano thabit kwa kutumia *Utengano* (1980). Pia utafiti huu ulifanikiwa kutoa maarifa juu ya namna juu ya namna bora ya kutumia mitindo kutoa kazi yenye uzito wa kiufundi. Mwisho kabisa utafiti huu ulijadili baadhi ya makossa ambayo hutendwa na watunzi wa kazi za fasihi wanapotumia mitindo mbalimbali. Kwa ufupi tunaweza kusema kwamba uchunguzi huu umejaribu kueleza namna bora ya kuwasilisha ujumbe katika tungo za ki riwaya. Kazi zote za riwaya ambazo hukosa ukubalifu wa watu mara nyingi chanzo ni kukosa kuwasilisha ujumbe katika namna stahiki. Hii hali mara nyingi huwa ni ishara ya mtafiti kukosa uahamu mwafaka juu ya matumizi bora ya mtindo.

## . 5.3 Mapendekezo

Utafiti huu ulijadili mada hii kadri ya uwezo wa mtafiti lakini hata tukijadili kwa undani kiasi gani hatuezi kumaliza kila kitu. Hivy basi, kazi hii haiwezi kushughulikia kila jambo linaloibuka chini ya kipengele hiki hata kama ni katika mipaka ya utafiti. Hivyo basi hapa tutapendekeza baadhi ya mambo ambayo tunaona kwamba haja ipo ya kuyashuhulikia.

### 5.3.1 Haja ya Kuangalia Matumizi Bora ya Vipengele Vingine

Kila mtu anauwezo wa kuandika na kutunga kazi ya kiasihi ila ni wachache tu ambao wanao uwezo wa kuandika kazi ya fasihi ya kiufundi. Hivyo basi ipo haja kubwa ya kuelimisha watu juu ya namna ya kutumia vipengele vingine vya kifani. Ninasema vya kifani kwa sababu fani kama sote tunavyofahamu ndio umbo la nje la kazi ya fasihi au fani ndio uhalisia wa fasihi kama inavyodhirika. Maudhui au umbo la ndani la afsihi yoyote ile haliwezi kudhihirika pasi na uwepo wa fani. Fani inajumlisha vipengele kama vile Jina, wahusika, mandhari, lugha, muundo na mtindo. Ila haina maana kwamba hakuna haja ya kusoma maudhui ila fani isipoeleweka kazi haiwezi kutokea vizuri ipasavyo. Isitoshe, katika mrngo huohuo ipo haja ya kupatikana kazi ambazo zinawafunza watu namna vipengele vya fani na maudhui vinavyo saidiana au kuchangiana katika kuleta ujumbe kwa hadhira lengwa.

### 5.3.2 Kuanda Wandishi Chipukizi

Makosa yakizidi katika kazi za fasihi au uwasilishaji mbaya wa ujumbe wa kiutafiti ukikithiri, Ukuaji wa fasihi unakufa na mwisho wa siku maendeleo ya fasihi ya lugha au jamii Fulani huzoroteka. Hali kadhalika inaweza kutokea katika fasihi ya Kiswahili. Iwapo zikikithiri kazi zilizojaa kasoro za uwasilishaji ujumbe mvuto wa fasihi utakufa mbele ya hadhira yote kwa ujumla jambo ambalo litaathiri pia wale wandishi wenye kazi nzuri.

## 5.4 Hitimisho

Mtindo kama kitambulisho kikuu cha msanii yeyote ule, lazima matumizi yake yaelezwe kwa wandishi wanaotarajiwa (chipukizi). Wahenga hawakukosea kudai kuwa samaki mkunje angali mbichi. Sio katika fikra tendekaji kudhani kwamba wandishi hao watakosolewa baada ya ubobezi wao katika fani hii ya uandishi. Utoaji mafunzo haya sio jambo hufanywa mara moja tu ukawa ndio mwisho wa kazi, bali mafunzo haya hupaswa kukaririwa na ikiwezekana kufanywa kuwa ni sharti mojawapo ya mtu kutambuliwa kama mwandishi mwenye kazi zinazopaswa kuzingatiwa. Hii ni kwa lengo la kudhibiti utoaji kazi zenye makossa yanayoweza kuepukika.

**Marejeo**


Senkoro, F.E.M.K (1982) Fasihi. Dar es salaam: Press and Publicity Centre.

Wamitila, K. (2003) Kichocheo cha Fasihi: Similizi na Andishi. Nairobi: Focus Books.

Wamitila, K. (2003) Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia. Nairobi: Focus Publishers Limited.

Leech, G. N. (1969). A Linguistic Guide to English Poetry. London: Longman Group Ltd.

Leech, G. N. na Short, M. (1981, 2007). Style in Fiction: A Linguistic Introduction to English Fictional Prose. 2nd Edition Harlow: Longman Group Ltd.

Ndung‟u, N. (1996). Uhakiki wa Fani katika Riwaya za Katama Mkangi: Ukiwa, Mafuta na Walenisi. Tasnifu ya M.A, (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Ongarora, S.O. (2007). Mtindo katika „Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine. ‟ Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.

Otieno, N. O. (2005) Muumano wa Leksia katika Matini: Babu Alipofufuka. Tasnifu ya M.A, (Haijachapishwa): Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kitali, H. N. (2011). Fani na Usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia za Pango na Mama Ee. Tasnifu ya (M.A). Chuo kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Katutu, R. M. (2013) Mtindo katika Diwani ya „Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine.‟ Tasnifu ya

Uzamili (M.A). Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Wafula, R. na Kimani, N. (2007). Nadharia za Uhakiki wa Fasihi. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. W. (2002). Uhakiki wa Fasihi: Msingi na Vipengele vyake. Nairobi: Phoenix Publishers.

http://lisakoski.hubpages.com/hub/Writing-styles-of-English-Literature.htm

Mohamed, S. A. (1980). Utengano. Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.

Mohamed, S. A. (2014). Kamwe si mbali tena. Nairobi: Oxford University Press.

BAKIZA, (2010). Kamusi la Kiswahili Fasaha, Nairobi: Oxford University Press.

Wales, Katie. "Kamusi ya Mitindo." Routledge, 1990, New York.

Burke, Michael, mhariri. "Kitabu cha Routledge cha Mitindo." Routledge, 2014, New York.

Barry, Peter. "Nadharia ya Mwanzo: Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi na Utamaduni." Manchester University Press, Manchester, New York, 1995.


Ukiushi Kama Elementi ya Kimtindo Katika Baadhi ya Riwaya za Ken Walibora